Ukusanyaji Takwimu na Utunzaji sahihi wa Kumbukumbu

- Eneo la mavuno na msimu
- Aina ya zana za uvuvi
- Tarehe ya uvunaji na saa
- Aina ya samaki wanaovuliwa
- Kiasi cha samaki waliovuliwa
- Namba ya Boti ya Uvuvi

Umuhimu wa Takwimu

- Kumwezesha mvuvi kupanga mipango muhimu ya kuratibu kipato cha mvuvi
- Kuiwezesha jamii kupanga mikakati ya uvunaji endelevu
- Kuiwezesha Serikali kupanga mipango ya ufuatiliaji na kutafuta ufumbuzi wa matatizo
- Kuiwezesha Serikali kupanga mipango ya maendeleo na usimamizi endelevu

Fursa za Usimamizi Endelevu na Utunzaji wa Raslimali za Uvuvi

- Ushiriki wa moja kwa moja katika kupanga mipango ya uvunaji endelevu
- Kuibuka kwa wadau wa maendeleo kusaidia mipango ya endelevu ya usimamizi
- Ushiriki wa utunzaji mazingira yanayozunguka raslimali za uvuvi
- Uratibu wa mipanga ya usimamizi katika ngazi za uongozi kuanzia serikali ya kijiji hadi serikali kuu.

Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

AFISA MFAWIDHI WA KANDA

NA MSIMAMIZI WA MRADI (TASP II)

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI NA VIWANGO KANDA YA ZIWA VICTORIA

S.L.P. 1213 MWANZA

SIMU

+255 28 2550864

+255 754/784 437234

Barua Pepe: nfqcl_mz@yahoo.co.uk

Tovuti: www.nfqcl.go.tz

Imetayarishwa na Maabara ya Kitaifa ya Samaki chini ya Mpango wa TASP II kwa ufadhili wa mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (EDF)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI NA VIWANGO

Rasilimali za Uvuvi

TRADE AND AGRICULTURE SUPPORT PROGRAMME II (TASP II)

Rasilimali za Uvuvi

Faida zake

- Ni chanzo cha chakula kwa binadamu
- Ni chanzo cha kipato na uchumi wa familia
- Ni chanzo cha dawa kwa binadamu

Aina na Zana Bora za Uvuvi endelevu

- Uvuvi wa Ndoano
- Uvuvi wa makila
- Nyavu ya kijika

Utangulizi

Rasilimali za Uvuvi ni maliasili zote zilizoko ndani ya Ziwa na Maeneo yanayowezesha ustawi wa samaki

Zana Bora

- Zana zilizohalalishwa kisheria kutumika katika muda au/na eneo muafaka.
- Nyavu za makila zaidi ya inchi 6, kutegwa na kuaguliwa sio zaidi ya masaa manane (8). Urefu wa kamba ya ndoano unatakiwa uwe chini ya nusu ya urefu kati ya kamba mbili za ndoano katika mgonzo.
- Ndoano size namba 9, 10 na 11.
- Nyavu za dagaa zenye macho yasiyopungua milimita 8.

Aina za Rasilimali

- Maji
- Viumbe katika maji
- Maeneo ya mazalia na makuzi ya samaki
- Mazingira ya ziwa/bahari

- Ni chanzo cha njia ya usafiri
- Ni maeneo ya utalii
- Ni eneo la burudani na michezo